# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# MWONGOZO MDOGO WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI

**Februari, 2022**

## 1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu mdogo ni ufafanuzi wa jinsi ya kukusanya taarifa za anwani za makazi. Mwongozo huu wa Ukusanyaji wa Taarifa za Anwani za Makazi umeandaliwa ili kumsadia mkusanya wa taarifa za Anwani katika Mitaa/Shehia/Vitongoji aweze kukusanya taarifa kwa usahihi kulinga na melekezo, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

## 2.0 WATUMIAJI WA MWONGOZO

Mwongozo huu utatumiwa na Mkoa/Wilaya/Halmashauri ili kupata uelewa wa namna ya kukusanya taarifa za Anwani za makazi katika maeneo yao. Pia mwongozo huu utatumiwa na Afisa /Mtaatalamu/ Mtu yeyote atakayeteuliwa na kuidhinishwa na Katibu Tawala wa Mkoa au Mkurugenzi wa Halamshauri husika kukusanya taarifa za Anwani katika Mtaa/Shehia/Kitongoji husika.

## 3.0 UTARATIBU WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI

Serikali inahakikisha ifikapo mwaka Mei, 2022 Halmashauri zote (Mjini na Vijiji) zitafikiwa na Mfumo wa Anwani za Makazi. Katika kufanikisha ukusanyaji wa taarifa za anwani za makazi, Programu tumizi ambayo inaitwa NaPA itatumika kukusanya taarifa. Programu tumizi hii itakuwa na Dodoso la Anwani za makazi, ambalo ndilo litakalo jazwa:-

## DODOSO LA ANWANI ZA MAKAZI

Limegawanyika katika sehemu kuu tano (5);

- Sehemu A: Usajili wa Taarifa za Anwani (Anwani Kuu)
- Sehemu B: Usajili wa Huduma
- Sehemu C: Usajili wa Taarifa za Anwani tegemezi
- Sehemu D: Usajili wa Taarifa za Mmiliki wa Anwani
- Sehemu E: Usajili wa Taarifa za Wategemezi wa Anwani

**SEHEMU A: USAJILI WA TAARIFA ZA ANWANI**

Sehemu hii inamtaka mkusanya taarifa kuchukua taarifa zote za anwani kuu (Jengo kuu au kiwanja endapo hakuna jengo). Taarifa za msingi ambazo karani lazima azichukue kwa usahihi ni pamoja na;- majira nukta, jina la barabara, namba ya Anwani, jina la anwani (kama lipo), namba ya kiwanja, kitalu na mahali (endapo kiwanja kimepimwa), Aina ya jengo na matumizi ya jengo au kiwanja.

**Angalizo:** Anwani inaweza kuwa na Jengo/Nyumba au kiwanja kitupu. Anwani yenye majengo inakuwa na Jengo kuu/Nyumba kuu moja, majengo mengine yanayokuwemo ndani ya anwani hiyo yatakuwa Anwani Tegemezi.

**Swali A1: Majira Nukta**

Hizi ni alama za utambulisho wa kijiografia wa eneo la jengo/kiwanja kilipo (Latitudo na Longitudo) kwenye uso wa dunia ambazo simu itazitafuta na kuzinakiri yenyewe.

**Swali A2: Usahihi**

Usahihi husaidia kutupa uhakika wa majira nukta ya eneo husika

**Angalizo:** Mkusanya taarifa utatakiwa kuwa makini katika kuangalia usahihi wa majira nukta yasiwe juu ya mita nne.

**Swali A3: Jina la Barabara/Kitongoji**

Mkusanya taarifa achague jina la barabara/kitongoji kutoka kwenye machaguo, na jina hilo liendane na jina la barabara/Kitongoji ambayo anachukua taarifa kwa wakati huo na liwe ni jina linalotambulika kwenye eneo husika.



**Swali A4: Namba ya Anwani**

Hii ni namba kamili inayoonekana mbele ya jengo kwenye kibao cha njano au iliyochorwa kwa wino kwenye ukuta wa nyumba, getini au mlangoni. Upande wa kushoto wa barabara utaona namba witiri ( 1, 3, 5, 7 na kuendelea) na upande wa kulia wa barabara utaona namba shufwa (2, 4, 6, 8, na kuendelea)

**Swali A5: Je Kuna Nguzo?**

Baada ya mkusanya taarifa kujaza namba ya Anwani atachagua iwapo kuna kibao cha njano au laa.

**Swali A6: Jina la Anwani**

Mkusanya taarifa atajaza jina la Anwani kama Anwani anayosajili ina jina. Mfano wa jina la Anwani ni kama vile; Mawasiliano Tower, Takwimu House

**Swali A7: Hadhi ya kiwanja**

Mkusanya taarifa atajaza hali ya upimaji kwenye eneo ambalo anwani imetolewa; kujua iwapo kiwanja kimepimwa au hakijapimwa.

**Swali A8: Taarifa za Upimaji**

Ikiwa imetambulika kuwa kiwanja kimepimwa mkusanya taarifa atajaza maelezo ya utambulisho wa kiwanja kulingana na hati au ramani ya upimaji kwa mujibu wa mipango miji ambapo atataja namba ya kiwanja, kitalu na mahali. Mfano: Namba ya kiwanja: 12, Kitalu: H, Mahali: Mtakuja

**Swali A9: Uwepo wa jengo**

Mkusanya taarifa atajaza jibu la swali hili kwa kuangalia iwapo kiwanja chenye anwani husika tayari kina jengo au ni kiwanja tupu.

**Swali A10: Aina ya ujenzi**

Lengo la swali hili ni kutaka kujua kama jengo lililopo ni la jadi au la kisasa. Mkusanya taarifa atatakiwa kuchagua aina ya ujenzi kwa kutizama aina ya ujenzi wa jengo alilolikuta kwenye Kiwanja.

**Swali A11: Aina ya jengo**

Lengo la swali hili ni kutaka kujua kama jengo lililopo ni la kawaida au ghorofa. Mkusanya taarifa atatakiwa kuchagua aina ya jengo kwa kutizama aina ya jengo alilolikuta kwenye Kiwanja.

**Angalizo:** Iwapo jengo ni ghorofa mkusanya taarifa atatakiwa kujaza idadi ya mbawa na idadi ya ghorofa.

**Angalizo:** Kwa Jengo lenye Mbawa chukua idadi ya ghorofa kutoka kwenye Mbawa yenye idadi kubwa ya ghorofa kuliko Mbawa zote.

**Swali A12: Matumizi ya jengo au kiwanja**

Mkusanya taarifa atabainisha matumizi ya jengo au kiwanja husika kwa kuangalia shughuli zinazofanyika katika jengo/kiwanja hicho. Baada ya kubainisha matumizi husika atachagua matumizi hayo kwenye machaguo.

**Mifano ya nyumba/majengo kwa picha**




Nyumba ya kawaida




Nyumba ya Ghorofa

**Mfano wa Ghorofa**




Ghorofa 2




Ghorofa 3



Ghorofa 4

**Mfano wa Mbawa**




Jengo hili lina mbawa tatu

**Angalizo:** Mbawa ni sehemu za jengo ambazo zimeshikana na kuunganishwa kwenye ghorofa.

**Mfano wa Majengo Tegemezi**



Anwani zenye Majengo tegemezi

**Mfano wa Jina la Anwani**



**SEHEMU B: USAJILI WA HUDUMA ZINAZOPATIKANA KWENYE ANWANI**

Sehemu hii inamtaka mkusanya taarifa kuchukua taarifa zote huduma zinazopatikana kwenye anwani husika.

**Swali B1: Aina ya Huduma**

Swali hili linataka uchaguwe aina ya huduma au shughuli zinazofanyika katika jengo/kiwanja ambapo unachukua taarifa za anwani. Shughuli hizo zinaweza kuwa za kibiashara au huduma za kijamii. Mfano; Zahanati, Shule, Chuo kikuu, Msikiti, Kanisa n.k

**Swali B2: Jina la Huduma**

Swali hili linataka mkusanya taarifa aandike Jina la huduma iliyopo kwenye jengo/kiwanja kwenye anwani husika. Mfano NMB Bank, Shule ya Sekondari Maendeleo n.k.

**Angalizo:** Endapo kwenye anwani hiyo kuna huduma zaidi ya moja mkusanya taarifa ataongeza huduma kwa kadri vilivyo kwenye anwani hiyo.

**SEHEMU C: USAJILI WA TAARIFA ZA ANWANI TEGEMEZI**

Sehemu hii inamtaka karani kujaza taarifa za Anwani tegemezi zote zinazopatikana kwenye anwani husika. Karani atajaza taarifa za anwani tegemezi endapo anwani husika ina majengo zaidi ya jengo kuu ambalo amelisajili awali.

**Swali C1: Aina ya jengo**

Lengo la swali hili ni kutaka mkusanya taarifa kujaza kama jengo lililopo ni ghorofa au kawaida. Endapo jengo ni Gorofa mkusanya taarifa atatakiwa kujaza Idadi ya Mbawa na idadi ya Ghorofa.

**Swali C2: Jina la Jengo**

Swali hili linamtaka mkusanya taarifa kujaza jina la jengo lililopo kwenye jengo tegemezi husika. Jina la jengo mara nyingi hupatikana kwenye majengo ya biashara. Majengo ya makazi hayana majina. Mfano wa jina la jengo ni Takwimu House, Benjamini Mkapa Towers, Mawasiliano tower n.k

**Swali C3: Matumizi ya jengo/kiwanja**

Mkusanya taarifa atabainisha matumizi ya jengo tegemezi husika aliyoyakuta kwa kuangalia shughuli zinazofanyika katika jengo tegemezi hilo. Baada ya kubainisha matumizi husika atachagua matumizi hayo kutoka kwenye ya orodha ya huduma.

**SEHEMU D: USAJILI WA TAARIFA ZA MMILIKI WA ANWANI**

Sehemu hii inamtaka karani kujaza taarifa za Anwani tegemezi zote zinazopatikana kwenye anwani husika. Karani atajaza taarifa za anwani tegemezi endapo anwani husika ina majengo zaidi ya jengo kuu ambalo amelisajili awali.

**Swali D1: Aina ya umiliki wa Anwani**

Swali hili linalenga kujua aina ya mmiliki wa anwani, mkusanya taarifa atachagua taarifa za wamiliki wafuatao;

1. Mmiliki Binafsi
2. Kampuni
3. Kikundi
4. Taasisi

**Aina ya umiliki wa Anwani (Kama ni Mmiliki Binafsi)**

Iwapo mmiliki ni mtu binafsi mkusanya taarifa ataanza kuchagua uraia wake; kama ni raia wa Tanzania, atamuuliza iwapo ana namba ya NIDA au laa. Kama mmiliki ana namba ya NIDA mkusanya taarifa ataijaza sehemu ya Namba ya NIDA na kubonyeza kitufe na kuvuta taarifa.

Kama mmiliki hana namba ya NIDA mkusanya taarifa atatakiwa kujaza taarifa za mmiliki ambazo ni:-

**Swali D2: Jina la kwanza**

**Swali D3: Jina la kati**

**Swali D4: Jina la ukoo**

**Swali D5: Tarehe ya kuzaliwa**

**Swali D6: Jinsi (Kama ni Mwanamke au Mwanaume)**

**Swali D7: Namba ya TIN, kama anayo**

**Swali D8: Taarifa ya kama anaishi kwenye hiyo anwani au laa**

**Swali D9: Biashara anazomiliki kwenye hiyo anwani, kama zipo**

**Swali D10: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Aina ya umiliki wa Anwani (Kama ni Kampuni)**

Iwapo mmiliki ni kampuni, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza namba ya usajili ya kampuni; baada ya kujaza mkusanya taarifa atajaza na kubofya kitufe kuvuta taarifa zifuatazo:-

**Swali D10: Jina la kampuni**

**Swali D11: Kifupisho cha jina la kampuni**

**Swali D12: Namba ya TIN**

**Swali D13: Huduma zinazomilikiwa na Kampuni kwenye hii anwani, kama zipo**

**Swali D14: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Aina ya umiliki wa Anwani (Kama ni Kikundi)**

Iwapo mmiliki ni kikundi, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza taarifa zifuatazo:-

**Swali D15: Namba ya usajili ya Kikundi**

**Swali D16: Jina la Kikundi**

**Swali D17: Kifupisho cha jina la Kikundi**

**Swali D18: Namba ya TIN**

**Swali D19: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Swali D20: Huduma zinazomilikiwa na Kikundi kwenye hii anwani, kama zipo**

**Aina ya umiliki wa Anwani (Kama ni Taasisi)**

Iwapo mmiliki ni taasisi, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza taarifa zifuatazo:-

**Swali D21: Namba ya usajili ya Taasisi**

**Swali D22: Jina la Taasisi**

**Swali D23: Kifupisho cha jina la Taasisi**

**Swali D24: Namba ya TIN**

**Swali D25: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Swali D26: Huduma zinazomilikiwa na Taasisi kwenye hii anwani, kama zipo**

**Angalizo:** Iwapo kuna mmiliki zaidi ya mmoja kwenye anwani husika, mkusanya taarifa atabonyeza kitufe cha kuongeza mmiliki na kujaza taarifa za mmiliki mwingine kulingana na idadi ya wamiliki kwenye anwani husika.

**SEHEMU E: USAJILI WA TAARIFA ZA WATEGEMEZI WA ANWANI**

Sehemu hii inalenga kukusanya taarifa za wategemeaji wa anwani husika. Kuna aina mbili za wategemeaji wa anwani ambazo ni: Wategemezi-ndugu na Wategemezi-wapangaji. Kundi la Wategemezi-wapangaji linaweza kuwa ni watu binafsi au taasisi/kikundi/kampuni. Karani utajaza wategemezi wote.

**Swali E1:** Aina ya wategemezi wa anwani

Swali hili linalenga kutambua aina ya wategemezi wanaotegemea anwani hiyo. Swali hili lina mageresho manne ambayo karani atachagua kulingana na uhalisia atakaoukuta wakati wa mahojiano. Wategemezi wa Anwani wanaweza kuwa watu binafsi (ndugu/wapangaji) au Kampuni/Taasisi/Kikundi (Wapangaji).

**Aina ya tegemezi wa anwani (Kama ni ndugu au mpangaji)**

Iwapo mtegemezi ni mtu binafsi mkusanya taarifa ataanza kuchagua uraia wake; kama ni raia wa Tanzania, atamuuliza iwapo ana namba ya NIDA au laa. Kama mtegemezi ana namba ya NIDA mkusanya taarifa ataijaza sehemu ya Namba ya NIDA na kubofya kitufe na kuvuta taarifa.

Kama mtegemezi hana namba ya NIDA mkusanya taarifa atatakiwa kujaza taarifa za mtegemezi ambazo ni:-

**Swali E2: Jina la kwanza**

**Swali E3: Jina la kati**

**Swali E4: Jina la ukoo**

**Swali E5: Tarehe ya kuzaliwa**

**Swali E6: Jinsi (Kama ni Mwanamke au Mwanaume)**

**Swali E7: Namba ya TIN, kama anayo**

**Swali E8: Taarifa kama anaishi kwenye hiyo anwani au laa**

**Swali E9: Biashara anazomiliki kwenye hiyo anwani, kama zipo**

**Swali E10: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Aina ya mtegemezi wa anwani (Kama ni Kampuni)**

Iwapo mtegemezi ni kampuni, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza namba ya usajili ya kampuni; baada ya kujaza mkusanya taarifa atajaza na kubofya kitufe kuvuta taarifa zifuatazo:-

**Swali E10: Jina la kampuni**

**Swali E11: Kifupisho cha jina la kampuni**

**Swali E12: Namba ya TIN**

**Swali E13: Huduma zinazomilikiwa na Kampuni kwenye hii anwani, kama zipo**

**Swali E14: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Aina ya mtegemezi wa Anwani (Kama ni Kikundi)**

Iwapo mtegemezi ni kikundi, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza taarifa zifuatazo:-

**Swali E15: Namba ya usajili ya Kikundi**

**Swali E16: Jina la kikundi**

**Swali E17: Kifupisho cha jina la Kikundi**

**Swali E18: Namba ya TIN**

**Swali E19: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Swali E20: Huduma zinazomilikiwa na Kikundi kwenye hii anwani, kama zipo**

**Aina ya mtegemezi wa Anwani (Kama ni Taasisi)**

Iwapo mtegemezi ni taasisi, mkusanya taarifa atatakiwa kuuliza na kujaza taarifa zifuatazo:-

**Swali E21: Namba ya usajili ya Taasisi**

**Swali E22: Jina la Taasisi**

**Swali E23: Kifupisho cha jina la Taasisi**

**Swali E24: Namba ya TIN**

**Swali E25: Mawasiliano (Namba ya simu na barua pepe)**

**Swali E26: Huduma zinazomilikiwa na taasisi kwenye hii anwani, kama zipo**

**Angalizo:** Iwapo kuna mtegemezi zaidi ya mmoja kwenye anwani husika, mkusanya taarifa atabonyeza kitufe cha kuongeza mtegemezi na kujaza taarifa za mtegemezi mwingine kulingana na idadi ya wategemezi kwenye anwani husika.

**HITIMISHO**

Ni vizuri mkusanya taarifa akasoma na kuuelewa vizuri huu mwongozo. Mwongozo huu utamsaidia kujua ni taarifa gani anaenda kukusanya na pia jinsi ya kuyajibu maswali ambayo yanatumika kupata taarifa.